HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

MPANGO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MSITU WA NYAMKONGOO

MPANGO HUU UMEANDALIWA NA SERIKALI YA KIJIJI CHA NYAMWAGE

2016

YALIYOMO

1: UTANGULIZI 4
1.1 Umiliki wa Msitu 4
1.2 Lengo Kuu la Mpango wa Usimamizi 4
1.3 Madhumuni 4
1.4 Mfumo wa Usimamizi 5
1.5 Muda wa Utekelezaji na Marekebisho ya Mpango 5
2: HISTORIA FUPI YA MPANGO WA USIMAMIZI WA MSITU 6
2.1 Maelezo Kuhusu Kijiji 6
2.1.1 Jamii 6
2.1.2 Hali ya Kiuchumi na Kijamii 6
2.2 Maelezo kuhusu Misitu 7
2.2.1 Vyanzo vya Maji 7
2.2.2 Hali ya Udongo 7
2.2.3 Uoto wa Asili na Mazingira. 7
2.2.4 Jamii za Miti ya Mbao 7
2.2.5 Mazao Yasiyotimbao 7
2.2.6 Wanyama Pori 8
2.2.7 Matumizi ya Mazao ya Msitu kwa wanakijiji 8
2.3 Maeneo Madogo ya Usimamizi. 8
2.4 Matumizi ya Msitu 8
2.4.1 Mambo ya Asili & Haki za Kijadi 8
2.4.2 Historia ya Nyuma 9
2.4.3 Matumizi ya Sasa 9
3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU. 10
3.1 Matumizi ya Msingi 10
3.2 Matumizi Huru ya Misitu 10
3.3 Shughuli katika Misitu Zitakazotozwa Ushuru 10
3.4 Mazao Yanayohitaji Vibali 10
3.4.1 Utaratibu wa Uvunaji Miti ya Mbao. 11
3.4.2 Mazao Mengine ya Misitu Yatakayokatiwa Leseni 12
3.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu 13
4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU 14
4.1 Kijiji 14
4.1.1 Haki 14
4.1.2 Manufaa 14
4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji 14
4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili 15
4.1.4.1 Mwenyekiti wa kamati ya maliasili 15
4.1.4.2 Katibu wa kamati ya maliasili 16
4.1.4.3 Mwekahazina wa kamati ya maliasili 16

4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji *16*
4.2 Halmashauri ya Wilaya 17
4.2.1 Haki *17*
4.2.2 Manufaa *17*
4.2.3 Majukumu *17*
4.3 Serikali Kuu 17
4.3.1 Majukumu *17*
4.4 Mashirika yasiyo ya Kiserikali 18
4.4.1 Majukumu *18*
5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU 19
5.1 Mikakati ya Jumla ya Kuendeleza Msitu 19
5.2 Ulinzi wa Msitu 20
5.2.1 Ushirikishwaji wa Jamii katika Ulinzi wa Msitu *20*
5.2.2 Walinzi wa Doria *20*
5.3 Kusafisha Mpaka na Barabara za Moto 20
5.4 Kurudisha hali ya Msitu 20
5.4.1 Kutokana na Machipukizi (Uoto wa asili) *20*
5.4.2 Upandaji wa miti kwenye maeneo yaliyo wazi *21*
5.4.3 Palizi kwenye maeneo yaliyopandwa miti *21*
6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU 22
6.1 Vyanzo vya Mapato 22
6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau 22
6.3 Matumizi ya Mapato 22
6.4 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha 22
6.4.1 Vitabu Muhimu vya Kutunza Kumbukumbu Vinavyotakiwa *23*
6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi *23*
6.4.3 Kuwajibishwa *23*
7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI 24
7.1 Ufuatiliaji 24
7.2 Tathimini ya Kati na ya Mwisho 24
UHALALI WA MPANGO 25
MPANGO WA USIMAMIZI MISITU 25
MAREKEBISHO YA MPANGO 25
KIAMBATISHO A : *RAMANI YA MISTU WA NYAMKONGO(NYAMWAGE)* 26
KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI 28
Kazi za Kila Mwaka *28*
- **KUHAKIKI MIPAKA YA MSITU. 28**
- **KUSAFISHA MIPAKA YA MSITU NA KULIMA BARABARA ZA KUZUIA MOTO 28**
- **KUDHIBITI UCHOMAJI MOTO OVYO MSITUNI; 28**

Kazi za Mwaka wa Pili *29*
Kazi za Mwaka wa Tatu *30*
Kazi za Mwaka wa Nne *30*

Kazi za Mwaka wa Tano.....*30*

KIAMBATISHO C : VIWANGO VYA USHURU.....**30**

SURA YA KWANZA

1: UTANGULIZI

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa Misitu. Pia sera inasisitiza mchango wa sekta ya Misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Mwaka 2002 Serikali ya Tanzania ilipitisha sheria mpya ya Misitu ambayo inaipa mamlaka jamii zinazoishi kandokando ya Misitu kusimamia Misitu yao. Kijiji cha Nyamwage kimeandaa mwongozo wa matumizi endelevu wa Misitu ya Kijiji. Matumizi haya yameainishwa katika mpango huu.

Mpango huu ni mwongozo wa shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi cha kutumika kwa mpango na shughuli hizo zimefafanuliwa na kuwekwa bayana. Shughuli hizo ni uboreshaji wa Misitu, kuanzisha utaratibu wa usimamizi, udhibiti wa uvunaji haramu, usimamizi wa sheria za Misitu,ukusanyaji na usimamizi wa mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali za Msitu. Kutakuwa na utunzaji wa kumbukumbu za shughuli zote zilizofanyika ili kuendana na matakwa ya mpango. Kumbukumbu zote zitapatikana pia katika Halmashauri ya Wilaya. Sheria ndogo zitatungwa ili kusimamia utekelezaji wa mpango.

Mpango huu umeandaliwa na Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Nyamwage, timu ya wawezeshaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kushirikiana na shirika la MCDI na WWF chini ya Mpango wa Taifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mpango huu utatumika katika kipindi cha miaka mitano cha Umiliki wa Misitu

.

1.1 Umiliki wa Msitu

Kijiji cha Nyamwage kinamiliki Msitu ya Nyamkongo Misitu hii ilitengwa kuwa Misitu ya hifadhi ya Kijiji cha Nayamwage mwaka 2006 chini ya usaidizi wa wataalamu toka Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na wawezeshaji wa Mradi wa Misitu ya Ukanda wa Pwani chini ya shirika la WWF.

1.2 Lengo Kuu la Mpango wa Usimamizi

Msitu ya Nyamkongo ilitengwa kwa lengo la kulinda, kuhifadhi na kufanya uvunaji endelevu kwa kuvuna mazao ya mbao, mazao yasiotimbao na rasilimali zingine za Misitu kiendelevu. Lengo kuu likiwa ni kuweka Msitu katika hali ya uasilia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho.

1.3 Madhumuni

Kuboresha hali ya maisha ya wanajamii wa Kijiji cha Nyamwage kwa;

- Kuhifadhi eneo lenye ukubwa wa hekta 1644.4 la Msitu wa Nyamkongo dhidi ya ukataji miti ovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.
- Kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mazao yasiyo timbao kwa wakati wote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
- Kijiji cha Nyamwage kupata mapato kutokana na biashara ya rasilimali za Misitu ili kuboresha maisha ya wanakijiji wake.

1.4 Mfumo wa Usimamizi

Usimamizi misitu ya asili unaofuata uvunaji endelevu, upandaji wa miti ya asili na utunzaji wa machipukizi na udhibiti wa moto kwa kufuata mpango uliopo.

1.5 Muda wa Utekelezaji na Marekebisho ya Mpango

i) Mpango huu utadumu kwa kipindi cha miaka mitano, lakini unaweza kupitiwa upya na kufanyiwa maboresho katika kipindi cha mwaka wa pili wa utekelezaji, au muda wowote itakapoonekana inafaa.

ii) Baada ya kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji, mpango huu utafanyiwa maboresho/marekebisho

iii) Mapendekezo ya Maboresho yataandaliwa na kujadiliwa na Kamati ya Maliasili, na kuwasilishwa kwenye Halmashauri ya kijiji, na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

iv) Kamati ya Maliasili na Halmashauri ya kijiji wanapaswa kushauriana na Afisa Misitu Wilaya, na/au wadau wengine wa maswala ya misitu, kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu wa kijiji kwa ajili ya kupitishwa na mkutano mkuu.

v) Afisa Mtendji wa kijiji akishirikiana na Kamati ya Maliasili, ataandaa taarifa za mabadiliko ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu, na kuziaambatanisha na muhtasari wa Mkutano mkuu wa kijiji uliothibitisha mabadiliko hayo, na kuziwasilisha katika Ofisi ya misitu ya Wilaya.

SURA YA PILI

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO WA USIMAMIZI WA MSITU

2.1 Maelezo Kuhusu Kijiji

2.1.1 Jamii

Kijiji cha Nyamwage kipo katika Kata ya Mbwara, Tarafa ya Muhoro katika Wilaya ya Rufiji. Kina idadi ya watu wapatao 4,939 (me 2,169 na ke 2,767) katika kaya zipatazo 1234 (sensa ya Mwaka 2012). Kila kaya ina wastani wa watu kati ya 4 na kina Hekta zipatazo 28,939.Kijiji hiki hapo zamani kilijulikana kwa jina la Nyamwage kutokana na wahamiaji toka Nyamsete na Ruambano kupaita sehemu inayomwaga maji toka mfereji wa Tawi. Nyaa mwage yaani mwaga maji kutokana na mvua nyingi. Kijiji hiki kinapakana na kijiji cha Ikwiriri kwa upande wa Kaskazini kilichopo kwenye Kata ya Ikwriri, kwa upande wa Mashariki kimepakana na Kijiji cha Chumbi C kilichopo katika Kata ya Chumbi, Magharibi kimepakana na Kitongoji cha Utunge kilichopo Kata ya Chemchem mji mdogo wa Utete, na kwa upande wa Kusini kimepakana na Tawi,Kusini-Mashariki kimepakana na Kijiji cha Mbwara kilichopo kata ya Mbwara..

Kijiji hakina cha Cheti cha Ardhi cha Kijiji kilichosajiliwa mwaka 2006 kwa mujibu wa upimaji wa mipaka ya vijiji mwaka 2006. Mipaka ya Kijiji imewekwa mawe ya kuonyesha alama za mipaka.

Vitongoji vya Kijiji vinavyotambulika ni:Nyamwage-Mashariki,Nyamwage-Magharibi na Shauri moyo. Kitongoji cha Nyamwage-Mashariki kipo karibu na Msitu wa Nyamkongo na kitongoji cha Nyamwage-Magharibi kipo karibu na msitu wa Yelya.

2.1.2 Hali ya Kiuchumi na Kijamii

Wanajamii walio wengi ni wakulima. Wengine hujishughulisha na uvuvi mdogo, ufugaji mdogomdogo, biashara ndogondogo,uvunaji wa mazao ya msitu na uchomaji mkaa.

Mazao makuu yanayozalishwa Kijijini ni;

- Mazao ya biashara ni ufuta,mbaazi na korosho.
- Mazao ya chakula ni mahindi, mpunga, mtama na jamii ya kunde(mbaazi,kunde na choroko).

Mapato yatokanayo na kilimo kwa kila kaya ni kati ya 800,000/- na 1,000,000/- kwa mwaka.

Huduma za jamii zinazopatikana Kijijini ni: Zahanati, Shule ya Msingi, Ofisi ya Serikali ya Kijiji, Misikiti, Makanisa, Visima vya maji na barabara.

Wananchi huteka maji toka kwenye visima virefu na mtandao wa maji ya bomba.

Wananchi hupata huduma za afya na za kijamii Mji wa Utete ambao unafikika kwa mwendo wa masaa sita kwa watembea kwa miguu, pikipiki dakika hamsini na gari mwendo wa dakika thelathini.Mji wa Muhoro unafikika kwa mwendo wa masaa mmoja na nusu,pikipiki kwa mwendo wa dakika kumi na mbili na gari ni mwendo wa dakika kumi saba. Mji wa Ikwiriri unafikika kwa mwendo wa masaa mmoja na nusu,pikipiki kwa mwendo wa dakika kumi na mbili na gari ni mwendo wa dakika kumi saba.

2.2 Maelezo kuhusu Misitu

Msitu wa Hifadhi ya Kijiji cha Nyamwage inajulikana kwa majina ya **Msitu wa Nyamkongo.** Jina la Nyamkongo limetokana na Bwawa lililozungukwa na miti ya Mkongo

Mahali ulipo Msitu na Ukubwa Wake

Msitu wa Nyamkongo una ukubwa wa Hekta 1644.4 na upo upande wa Mashariki kilomita tano toka Kijijini. Msitu wa Nyamkongo unapakana na barabara ya Kilwa upande wa Kaskazini, msitu wa akiba wa kijiji cha Nyamwage upande wa Magharibi , Kijiji cha Chumbi upande wa Mashariki na upande wa Kusini umepakana na Kijiji cha Mbwara.

Msitu wa Nyamkongo unafikika kwa kupitia barabara ya Mbwara na ya Kilwa na Matumizi ya maeneo yanayozunguka msitu wa Nyamkongo ni kama ifuatavyo;

- Upande wa kaskazini ni barabara ya Kilwa
- Upande wa kusini ni eneo la makazi na kilmo
- Upande wa magharibi ni eneo la shamba la miti la Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji
- Upande wa mashariki ni eneo la Msitu wa Chumbi

2.2.1 Vyanzo vya Maji

Vyanzo vya maji katika Misitu hii ni mabwawa ya msimu

- .Mabwawa ya msimu ambayo hutumika kwa manywesheo ya wanyama pori.

2.2.2 Hali ya Udongo

Aina ya udongo katika Misitu hii ni Tifutifu na Kichanga. Hali ya tabaka la udongo ni udongo wenye kichanga. Hali ya kijiografia ya Misitu ni tambarare katika maeneo makubwa

2.2.3 Uoto wa Asili na Mazingira.

Sehemu kubwa ya Misitu yote ni tambarare.

Uoto wa asili ni wa Miombo (Misitu ya mataji wazi) vichaka vya miti baada ya uvunaji mkubwa kufanyika miaka ya 1980 na uwanda wa misitu ya pwani

2.2.4 Jamii za Miti ya Mbao

Kuna aina nyingi za jamii tofauti za miti katika Misitu ya Kijiji. Baadhi ya Jamii ya Miti ya thamani ya mbao iliyopo msituni ni Mnepa, Mtondoro, Mlondondo, Mgongachuma, Mkarati, Mkuruti. Miti ya Mninga, Mkongo, Msekeseke, Mvule imevunwa kwa wingi sana.

2.2.5 Mazao Yasiyotimbao

Kuna aina mbalimbali za mazao yasiyo timbao kama vile Mianzi, uyoga, Ming'oko, Matunda pori na Majengo.

- Miti inayofaa kwa ujenzi ni ,Mtasi,Mtunda, Msekeseke.Mnepa
- Miti ya matunda ni ,Mtopetope,Mfuru,Mbuyu,Mkwaju,Ndaba

- Miti inayotumika kutengenezea kamba ni; Mchenga, Miombo, Mkebo na Mnepa.
- Miti inayotumika kwa dawa ni; Mkundekunde,Muangalaya,Mgogo na Mzizimia
- Jamii za uyoga zifuatazo zinapatikana katika Msitu huu Ulelema,Nguyuali,mbalape,nyakalomba.

2.2.6 Wanyama Pori

Orodha ya aina mbalimbali za wanyama pori wanaopatikana katika Msitu huu; Ngorombwe, Nyani, Tembo, Ndandala, Mbalapi, Ngiri, Nguruwe pori, Fungofungo, Chui,simba,fisi,nyati,punda,pofu,ndogolo,mbawala,kima,tumbili,Nyoka n.k.

Aidha Aina mbalimbali za ndege ambao hupatikana katika msitu ni ndege ngoma, kanga, kwale, chiriku, njiwa, tipitipi, kororo, njegea msitu, kinjochi n.k.

2.2.7 Matumizi ya Mazao ya Msitu kwa wanakijiji

Wanajamii wa Kijiji cha Nayamwage watatumia mazao ya Msitu kwa matumizi mbalimbali kama ujenzi. Mazao kama, Nguzo(kongowele), Fito kwa ajili ya ujenzi yanapatikana kwa wingi katika maeneo yaliyo jirani na makazi ya watu, hivyo kwa sasa wanakijiji hawategemei kupata mazao haya kutoka Misitu ya Kijiji bali yatakapokuwa yanahitajika yatakuwa bure kwa kibali/utaratibu maalumu.

2.3 Maeneo Madogo ya Usimamizi.

Misitu ya hifadhi ya Nymkongo umegawanyika katika maeneo madogo ambayo ni eneo la uvunaji na eneo ambalo uvunaji hautafanyika.

Eneo lenye ukubwa wa hekta 129 limetengwa kama eneo ambalo uvunaji hautafanyika katika msitu wa Nyamkongo. Uvunaji wa mazao ya Misitu hauruhusiwi kabisa katika maeneo haya. Maeneo haya yamependekezwa kwa ajili ya ufugaji wa nyuki wa kisasa kwa sababu ufugaji huu ni rafiki wa mazingira na hauambatani na uvunaji wa Miti wala uchomaji wa moto. Pia maeneo haya yamechaguliwa kama maeneo ambayo uvunaji haufanyiki kwa sababu yana uoto unao wakilisha hali ya Misitu mizima na ni makazi na mazalia ya wanyama zaidi ikiwa wanyama aina ya Nyani, Kima, mbawala,n.k.

Pia ndani ya msitu kuna misitu ya ukanda wa pwani (Misitu iliyofunga na isiyopukutisha majani kwa kipindi cha mwaka mzima na kuwa haiungui moto kwa sababu hakuna nyasi nyingi) eneo hili litaruhisiwa kuvumwa lakini kwa utaratibu wa kutambua maeneo yaliyofanyiwa uvunaji kwa kuchukua alama za GPS na eneo lenye miti zaidi ya mitatu yenye sifa za uvunaji mti mmoja utavunwa. Maeneo haya hayajaonyeshwa kwenye ramani ya msitu wa Kijiji lakini yanatambulika.

Asilimia 90 ya eneo lote la msitu ni eneo la uvunaji ambapo miti ya mbao yenye thamani itafanyiwa tathimini na kuandaliwa mpango wa uvunaji endelevu. Uvunaji endelevu wa miti itakayofanyiwa tathimini utafanyika katika eneo hili kwa kufuata mpango wa uvunaji ulioandaliwa

2.4 Matumizi ya Msitu

2.4.1 Mambo ya Asili & Haki za Kijadi

Msitu huu hauna maeneo yanayotumika kwa mambo ya kimila na kijadi japo maeneo hayo yanapatikana katika sehemu tofauti nje ya Msitu.

2.4.2 Historia ya Nyuma

Mwanzoni Misitu hii ilikuwa ni eneo tu la Kijiji watu walikuwa wanaishi na walikuwa wakilima Msituni, baadae ukaanza kuvunwa kiholela na wavunaji binafsi, kuwinda wanyama na kurina asali.

2.4.3 Matumizi ya Sasa

Msitu huu kwa sasa ni Msitu wa Hifadhi ya Kijiji ambapo Kamati ya Maliasili ndio meneja wa usimamizi wa Msitu. Matumizi ya sasa yatakayofanyika katika Misitu ya kijiji cha Nyamwage ni; ufugaji wa nyuki, uvunaji endelevu, uhifadhi wa vyanzo vya maji na bionuwai na matumizi ya mazao yasiotimbao na uokotaji wa kuni kavu yanayofuata utaratibu uliopangwa na Kijiji.

SURA YA TATU

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU.

Msitu utasimamiwa kama Msitu wa asili na kutakuwa na mabadiliko kiasi katika usimamizi huo ili kuepuka kubadilisha hali ya uasilia wa Msitu. Taratibu za kuingia Msituni na za matumizi ya mazao ya Misitu zimeelezwa katika Sheria ndogo za Usimamizi wa Msitu wa kijiji cha Nyamwage. Wale ambao hawatafuata taratibu hizi watatozwa faini kulingana na Sheria ndogo za usimamizi wa misitu za kijiji cha Nyamwage.

3.1 Matumizi ya Msingi

Wanajamii wa Kijiji cha Nyamwage watakuwa na haki ya kuingia katika Misitu ya Kijiji bila kibali na kupita njia zinazofahamika, haki hii itahusu Vijiji jirani vya Chumbi, Mbwara na Tawi bila kuathiri mazingira ya msituni.

Wanajamii pia watakuwa na haki ya kuchota maji katika mabwawa yaliyopo Misituni.

3.2 Matumizi Huru ya Misitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Nyamwage yatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyo timbao kama vile uyoga, matundapori, mbogamwitu, kuni, nyasi na madawa ya asili, vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure toka Kamati ya Maliasili kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kijiji. Wasio wakazi wa Kijiji cha Nyamwage wanaweza pia kuomba kibali toka Kamati ya Maliasili ya Kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu. Kamati ya Maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao haya yanatumiwa kiendelevu. Watumiaji wa nje ya Kijiji wanaotaka kuvuna mazao haya kwa ajili ya biashara watatozwa ushuru kama ilivyopangwa na Kamati ya Maliasili.

.

3.3 Shughuli katika Misitu Zitakazotozwa Ushuru

Kutakuwa na ushuru wa Serikali ya Kijiji kwa shughuli zifuatazo msituni;

- Kurina asali kwa kufuata taratibu kwa vikundi visivyo vya kijiji na watu binafsi.
- Kutembelea Msitu kwa ajili ya mafunzo.
- Utafiti.
- Utalii Msituni.

Viwango vya ushuru vimeonyeshwa katika **Kiambatisho C**. Watalaam na wawezeshaji ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia kufanikisha kwa mpango huu hawatahusika na kutozwa ushuru.

3.4 Mazao Yanayohitaji Vibali

i) Uvunaji wa mbao na ukataji wa majengo kwa ajili ya biashara utaruhusiwa kwa kibali cha kulipia.

ii) Kabla ya kuvuna jamii yeyote ya miti tathmini lazima ifanyike ili kubaini kiasi kilichopo na Mpango wa Uvunaji utatayarishwa.

iii) Tathmini hiyo itafanyika kufuatana na mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya rasilimali za misitu ya Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii au miongozo mingine inayotambulika na inayozingatia uendelevu.

iv) Taarifa ya Tathmini shirikishi ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini. Taarifa hizo zimetumika kuandaa mpango wa uvunaji endelevu.

v) Mpango huo unaelezea namna kiwango cha uvunaji kilivyopatikana kutokana na matokeo ya tathmini na unabainisha ni kwa namna gani kiwango hicho ni endelevu.

vi) Mpango wa uvunaji ni lazima uandaliwe na kamati ya maliasili na kuidhinishwa na Afisa Misitu wa Wilaya na kuambatanishwa katika mpango huu.

vii) Ujazo wa miti utakaovunwa kwa mwaka utazingatia kiasi cha ujazo wa miti kilichopo, bila kuathiri kiasi cha kuvuna mwaka unaofuata, kwa kuzingatia kiasi kilichopo kwa kipindi chote cha miaka mitano. Mbali na jamii za miti zilizoorodheshwa katika kipengele 2.2.5 hapo juu, hakuna jamii nyingine ya miti itavunwa kwa ajili ya biashara kabla tathimini na uandaaji wa mpango wa uvunaji endelevu wa rasilimali hizo kufanyika.

viii) Kama Kijiji cha Nyamwage kitahitaji kuruhusu uvunaji wa jamii ambazo hivi sasa hazikufanyiwa tathimini, itabidi Kijiji kiandike barua ya maombi ya kuvuna kwa Afisa Misitu wa Wilaya ya Rufiji.

ix) Kabla ya kuidhinisha uvunaji; Afisa Misitu wa Wilaya ya Rufiji atajiridhisha kama Tathimini ya kina na mpango wa uvunaji kwa ajili ya jamii hizo umefanyika. Kama tathmini haijafanyika Afisa Misitu kwa kusaidiana na kijiji watafanya tathimini na kuandaa mpango wa uvunaji.

x) Baada ya kupata kibali cha maandishi toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya kijiji kinaweza kufanya uvunaji wa miti hiyo.

3.4.1 Utaratibu wa Uvunaji Miti ya Mbao.

- Utaratibu huu utahusisha miti yote iliyofanyiwa tathmini na kuandaliwa mpango wa uvunaji endelevu.
- Uvunaji utafanyika kwa kufuata Mwongozo wa uvunaji katika misitu ya vijiji wa mwaka 2013 uliotolewa na Wizara ya Malaisili na Utalii.
- Mtu yeyote anayetaka kuvuna mazao ya Misitu toka Msitu wa Kijiji lazima kwanza aandike barua ya maombi Kijijini na aonyeshe aina na kiasi anachotarajia kuvuna. Pia atajaza fomu ya Maombi ya uvunaji na lazima awe amekidhi masharti ya Kuwa mfanyabiashara wa mazao ya Misitu kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za uvunaji.
- Kamati ya Maliasili wakishirikiana na Serikali ya Kijiji watajadili na kupitisha ombi hilo endapo wataridhia kufuatana na matakwa ya mpango wa usimamizi na mpango wa uvunaji wa Msitu tu. Kama mpango wa uvunaji haujaandaliwa kibali hakitatolewa na uvunaji hauruhusiwi.
- Kama bei haijaainishwa katika mpango wa uvunaji, Kamati ya Maliasili itapanga bei ya kuvuna mazao ya Misitu na bei hizo kupitishwa na Serikali ya Kijiji lakini bei itakayopangwa isiwe chini ya kiwango kilichowekwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002.
- Kamati ya Maliasili wakishirikiana na Serikali ya Kijiji pamoja na Afisa Misitu wa Wilaya watapanga bei ya mabaki yaliyoachwa Msituni baada ya uvunaji.
- Wanakijiji wa Kijiji cha Nyamwage watakaohitaji mbao kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ndani ya kijiji cha Nyamwage, watalipia asilimia hamsini (50%) ya bei

iliyoelekezwa na Serikali kwa kila mita moja ya ujazo . Fursa hii ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba Kijijini Nyamwage tu.

- Kamati ya Maliasili itafanya uhakiki wa eneo nyumba inapojengwa na kiasi cha mbao/miti inayohitajika, kabla ya kuidhinisha Maombi ya uvunaji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa wakazi wa Kijiji cha Nyamwage ndani ya Kijiji
- Kamati ya Maliasili itapaswa kutoa taarifa za kila mwezi zinazoonesha Jina la mkazi, kitongoji anachotoka na aina na kiasi cha miti alichopewa mkazi wa Kijiji aliyeruhusiwa kuvuna kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, thamani halisi ya miti hiyo kuendana na bei elekezi ya Serikali, na kiasi halisi (yaani 50%) ambayo mwanajamii amelipa. Taarifa hizi lazima zibandikwe kwenye mbao za matangazo na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu unaofuata
- Mwombaji atalipa gharama za ujazo wa mti mzima uliosimama aliyoomba kwa Kamati ya Maliasili na kupatiwa stakabadhi halali ya malipo na kibali cha uvunaji kinachoonesha ujazo aliomba na muda au kipindi cha kufanya uvunaji huo. Kamati ya maliasili itabaki na nakala moja ya kibali hiki.
- Mwombaji atawasilisha stakabadhi ya malipo pamoja na nakala ya kibali kwa Afisa Misitu wa Wilaya ya Rufiji ambaye atazipitisha na kumruhusu kuendelea na taratibu zingine za uvunaji. Pia, atatakiwa kulipa ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.
- Baada ya Afisa Misitu kujiridhisha Mwombaji atarudi tena Kijijini na ambapo Kamati ya Maliasili itamwonesha eneo la kuvuna mazao ya Misitu anayolipia na pia watasimamia zoezi la uvunaji wakiongozwa na msimamizi wa uvunaji.
- Kamati ya Maliasili watapima magogo yote yaliyovunwa na kutafuta ujazo wake, nakala ya vipimo hivi itatolewa kwa Afisa Misitu wa Wilaya kwa uhakiki zaidi kabla ya kwenda kugonga magogo nyundo.
- Baada ya kuvuna, magogo yote yaliyokatwa na visiki yatagongwa nyundo.
- Mwisho mwombaji lazima apate kibali cha kusafirishia mazao yake toka kwa Ofisi ya Wilaya ya Wakala wa Huduma za Misitu. Mvunaji lazima awasilishe Kibali cha kusafirishia kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kamati ya Maliasili ili kuweka kumbukumbu ya namba ya kibali kabla mazao hayajatolewa Kijijini.
- Utaratibu huu utafuatwa kwa ununuzi wa mabaki ya magogo, vilingu na mazao mengine ya misitu yatakayovunwa kibiashara.

3.4.2 Mazao Mengine ya Misitu Yatakayokatiwa Leseni

- Kijiji hakitaruhusiwa kutoa leseni au vibali vya uwindaji wa Wanyamapori, vibali na leseni zote za uwindaji zitatolewa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya au serikali Kuu.

Taarifa ya tathmini shirikishi ya Msitu wa Mbumbila wa msitu wa hekta 1,294

Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu	**Miti ya Kati (Idadi)**	**Miti MiKubwa (Idadi)**	**Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu kwa Kipindi cha Miaka 5 (m3)**	**Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu kwa mwaka (m3)**
Mtondoro	1180	20	2717	543.4
Msufi pori	111	0	317	63.4
Mlondondo	74	0	90	18

Mkuruti	86	0	123	24.6
Mnangu	383	0	777	155.4
Mnepa	51	0	78	15.6
Miombo	266	0	573	114.6
Mkongo	27	0	66	13.2
Mninga jangwa	22	0	40	8

3.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu

- Kilimo ndani ya Msitu;
- Kukata kuni mbichi;
- Kubangua asali;
- Kutega wanyama;
- Kuchimba mawe, mchanga au udongo kwa ajili ya biashara;
- Uchakataji wa mbao na magogo kwa kutumia misumeno ya moto;
- Kuchuna magome ya miti kwa ajili ya mizinga ya kienyeiji;
- Kulisha mifugo ndani ya Msitu;
- Makazi ndani ya Msitu;
- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijafanyiwa tathimini ya uvunaji endelevu;
- Uvunaji katika eneo la asilimia kumi (10%)
- Kuchoma moto ovyo;
- Uanzishwaji wa njia mpya zisizo rasmi ndani ya Msitu;
- Utengenezaji wa mkaa na
- Uwindaji wa wanyama bila kibali.

SURA YA NNE

4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU

Misitu ya Kijiji cha Nyamwage una wadau wafuatao; Serikali ya Kijiji, Wanakijiji, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Serikali Kuu, Mashirika (wahisani) na wadau wengine. Majukumu ya kila mdau yameelezewa kama ifuatavyo:

4.1 Kijiji

4.1.1 Haki

- Kumiliki na kutunza Misitu ya Kijiji.
- Kukamata, kutoza faini au kumshitaki mtu yeyote anayeenda kinyume na sheria ndogo za kijiji zilizopitishwa na mpango huu kisheria.
- Kutumia rasilimali kama ilivyobainishwa katika mpango wa Usimamizi wa Misitu.
- Kukusanya na kutumia ushuru na mapato mengine yatokanayo na mazao ya Misitu katika shughuli za maendeleo ya jamii na hivyo kuboresha hali za maisha ya wanajamii.
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya Misitu kwa kufuata sheria, sera na miongozo ya Misitu.

4.1.2 Manufaa

- Kutumia mazao ya misitu kwa matumizi ya nyumbani bila mashariti magumu kama ilivyoainishwa katika mpango wa usimamizi misitu;
- Kutumia miti na mbao kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa huduma za jamii Kijijini;
- Mapato yatokanayo na faini na ushuru wa mazao ya misitu ni mali ya Kijiji ingawa kunaweza kuwa na makubaliano ambapo Halmashauri ya Wilaya itapata gawio fulani kutokana na huduma za uwezeshaji kama ilivyobainishwa katika kipengele 7.2
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya Msitu kwa kufuata sheria, sera na miongozo ya Misitu.

4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji

- Msimamizi mkuu wa shughuli zote za utunzaji wa Msitu.
- Kudhibiti mapato na matumizi yote yatokanayo na Msitu.
- Kutatua migogoro inayohusiana na Misitu pale inapojitokeza na kupeleka matatizo hayo ngazi ya Halmashauri ya Wilaya pale yanaposhindikana kutatua Kijijini.
- Kutunga, Kuboresha na Kusimamia utekelezajki wa sheria ndogo na Mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Kijiji .
- Kuhakiki vibali vyote vilivyotolewa na Kamati ya Maliasili.
- Kupokea taarifa za uharibifu wa Msitu toka Kamati ya Maliasili na wanakijiji kwa ujumla na kuzifanyia kazi.

- Kujadili na kupitisha mipangokazi na bajeti ya mwaka ya Msitu wa Kijiji iliyoandaliwa na Kamati ya Maliasili.
- Kujadili na kuidhinisha mapendekezo ya matumizi yote ya fedha kwa Kamati ya Maliasili na Kikosi cha doria kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi ikiwemo miradi ya maendeleo ya Kijiji
- Kutoa taarifa ya matatizo yanayohusiana na utunzaji wa Misitu katika Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) na Halmashauri ya Wilaya
- Kushirikiana na wadau wengine katika utunzaji na usimamizi wa misitu.

4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili

Kamati ya Maliasili ina majukumu yafuatayo:

- Kuratibu shughuli zote za Msitu kama vile; Upandaji miti, ukusanyaji wa mazao ya Misitu na kutunza kumbukumbu za Msitu (Kamati ya Maliasili ndiyo Meneja wa Msitu)
- Kutoa vibali vya uvunaji wa mazao ya Misitu.
- Kuhakikisha doria imefanyika kila mara na kwa uhakika.
- Kuandaa mpango wa kazi wa mwaka wa shughuli za Msitu.
- Kutathmini rasilimali za Misitu na kutengeneza mpango wa uvunaji.
- Kutoa taarifa za maendeleo na uharibifu wa Msitu kwa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia na kufuatilia uvunaji.
- Kupendekeza na kusimamia sheria ndogo ikiwemo kuzirekebisha inapohitajika.
- Kuijulisha jamii juu ya matukio katika Msitu wa Kijiji na maeneo yanayozunguka.
- Kuielimisha jamii juu ya mabadiliko ya miongozo mbalimbali ya utunzaji Misitu.
- Kutoa taarifa ya robo, nusu na mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa Misitu kwa Serikali ya Kijiji na Afisa Misitu wa Wilaya.
- Kuhamasisha ushiriki wa wanakijiji katika uhifadhi wa Msitu
- Kufanya vikao vya Kamati ya Maliasili kila mwezi.
- Kujua mipaka ya Msitu na kuilinda.

4.1.4.1 Mwenyekiti wa kamati ya maliasili

- Kusimamia shughuli zote za Kamati ya Maliasili ikiwa ni pamoja na vikao
- Kuitisha mikutano ya Kamati ya Maliasili.
- Kuwa msemaji mkuu wa Kamati.
- Kusaini muhitasari yote ya vikao vya Kamati.
- Kuhakikisha Katibu anaandaa taarifa za maliasili na kuwasilisha katika Serikali ya Kijiji na Halmshauri ya Wilaya, pia kuweka kumbukumbu sahihi za vibali, mipango kazi, taarifa za mrejesho, mapato na matumizi, doria na faini
- Kutoa taarifa za mafanikio na matatizo ya ulinzi wa Msitu na shughuli zingine za Kamati Maliasili

- Atakuwa ni kiungo kati ya Kijiji chake na Kijiji vingine vinavyopakana na Msitu na atawezesha ushirikiano kati ya Afisa Misitu wa Wilaya, wadau wengine wa maliasili na wanakijiji

4.1.4.2 Katibu wa kamati ya maliasili

- Kuweka kumbukumbu za Kamati ya Maliasili
- Kuandaa ajenda za mikutano
- Kuandika mihutasari ya vikao vinavyofanywa na Kamati ya Maliasili
- Kutoa taarifa za Kamati kwenye Serikali ya Kijiji
- Kuandika na kutoa vibali vya uvunaji baada ya kupitishwa na Serikali ya Kijiji
- Kuratibu shughuli za doria.
- Kuwaalika wajumbe kwenye mikutano baada ya kuwasiliana na mwenyekiti
- Kusoma taarifa za mapato na matumizi ya Kamati.
- Kutekeleza shughuli zingine zozote atakazo agizwa na Kamati kupitia mwenyekiti.

4.1.4.3 Mwekahazina wa kamati ya maliasili

- Kutunza vitabu vya kumbukumbu za fedha za Kamati
- Kuandaa na kuwasilisha taaarifa za mapato na matumizi kwa Kamati ya Mailiasili kila mwezi
- Kupokea mapato yanayotokana na mazao ya Msitu na kutoa stakabadhi
- Kusaini stakabadhi na risiti zote zinazohusiana na malipo ya fedha.

4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji

- Kuzuia uharibifu wowote utakaojitokeza katika Msitu kama vile uchomaji moto na uvunaji holela wa mazao ya Misitu.
- Kutoa taarifa ya uharibifu wa aina yeyote utakaofanyika ndani ya Msitu kwa Kamati ya Maliasili na Serikali ya Kijiji.
- Kushiriki katika shughuli zote za kuboresha Msitu.
- Kupitia na kuidhinisha inapofaa sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili.
- Kushiriki katika kulinda Msitu na kutoa msaada kwa timu ya doria mara kwa mara.
- Kupitia, kuboresha na kuidhinisha mpango wa usimamizi wa Msitu na sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili na Halmashauri ya Kijiji;
- Kupokea au kudai na kujadili taarifa zinazohusu maendeleleo ya Msitu, mapato na matumizi na baadae kupitisha au kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maliasili na
- Kushiriki katika kulinda Msitu na kutoa msaada kwa timu ya doria mara kwa mara.

4.2 Halmashauri ya Wilaya

4.2.1 Haki

- Kupokea taarifa za mwezi, robo na nusu mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa Msitu.
- Kukagua vitabu vya mapato na matumizi na kuchukua hatua zinazotakiwa kama italazimu.
- Kurudisha mamlaka ya usimamizi wa Msitu chini ya Halmashauri ya Wilaya kama Kijiji kitashindwa kuusimamia ipasavyo.

4.2.2 Manufaa

- Kupungua kwa gharama za usimamizi wa Misitu;
- Kuongeza pato la halmashauri ya Wilaya kupitia mchango wa hiari wa kijiji wa 5% ya mapato yote yatakayotokana na Msitu wa Kijiji.
- Kuongeza pato la Halmashauri ya Wilaya kupitia ushuru wa 5% ya malipo anayofanya mnunuzi Kijijini.
- Kuboreka kwa usimamizi wa misitu na hivyo kudhibiti ufyekaji wa Misitu na kupunguza uharibifu wa Misitu;
- Kupungua kwa migogoro na migongano inayohusiana na matumizi ya Misitu kati ya Halmashauri ya Wilaya na jamii, na
- Kupungua kwa gharama za kusaidia vijiji baadhi ya miradi ya maendeleo pale Kijiji kinapopata mapato yanayotosha kutekeleza shughuli hizo.

4.2.3 Majukumu

- Kupitisha Mpango wa Usimamizi Misitu, Sheria ndogo na Mpango wa uvunaji.
- Kuhalalisha mazao yatokanayo na Msitu wa Kijiji.
- Kutoa watalaam kwa ajili ya shughuli za msitu pale inapohitajika.
- Kusaidia kutafuta soko la mazao ya Misitu.
- Kusimamia na kutatua migogoro ambayo iko juu ya uwezo wa Serikali ya Kijiji.
- Kuongoza zoezi la kubaini fursa na vikwazo katika kipindi cha kwanza na cha mwisho cha mpango huu.
- Kuingilia kati kama kuna jambo au shughuli yeyote imefanyika kinyume cha utaratibu wa mpango kazi.
- Kufuatilia na kushauri au kuchukua hatua wakati wote wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa Msitu na mpango wa uvunaji wa Msitu;
- Kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na Misitu yanatumika vizuri na Kijiji kama ilivyopitishwa na Mkutano mkuu wa Kijiji.

4.3 Serikali Kuu

4.3.1 Majukumu

- Kutoa watalaam washauri pale wanapohitajika.

- Kutunga Sheria, Sera na kutoa miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi misitu.

4.4 Mashirika yasiyo ya Kiserikali

4.4.1 Majukumu

- Kutafuta masoko ya mazao ya Msitu
- Kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa Msitu
- Kutoa msaada wa kitaalamu na kusaidia uendeshaji wa shughuli za kuendesha Msitu
- Kuwezesha kufanya tathimini za rasilimali za Misitu pale itakapohitajika
- Kufuatilia na kutoa ushauri wa utekelezaji wa shughuli za kuendeleza Msitu

SURA YA TANO

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU

Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na upandaji wa miti na utunzaji wa machipukizi dhidi ya moto, ulinzi wa Msitu, kinga na udhibiti wa moto pamoja na mipango ya muda mrefu ya matumizi endelevu ya mazao ya misitu. Mwongozo wa mpango wa utekelezaji wa miaka mitano umeoneshwa katika **kiambatisho B**.

5.1 Mikakati ya Jumla ya Kuendeleza Msitu

Katika kuendeleza Msitu, mikakati ifuatayo imewekwa;

- Kuelimisha jamii kuhusu madhara ya moto na Kudhibiti vitendo vya uchomaji moto ovyo Msituni.
- Kudhibiti malisho ya mifugo Msituni
- Kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti uvunaji holela na uharibifu mwingine wa Msitu.
- Kuhakiki mipaka ya Msitu.
- Kuelimsha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza Msitu
- Kuweka alama za kudumu kwenye mipaka ya Msitu mfano kupaka misitu rangi na kuweka mabango
- Kutoa elimu kwa Kamati ya Maliasili.
- Ubabuaji wa Msitu
- Kuhamasisha jamii kupanda miti
- Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo na mpango wa usimamizi wa Msitu (Serekali ya Kijiji)
- Kufungua akaunti ya Kamati ya Maliasili.
- Kukusanya mapato yanayotokana na Msitu (Kamati ya Maliasili)
- Kununua vitendea kazi vya Kamati ya Maliasili.
- Kukuza ushirikiano na Vijiji vingine juu ya uhifadhi wa Misitu
- Kuweka mpango mzuri wa Kamati mpya kuwa na uwakilishi wa Kamati ya zamani.
- Kuwezesha urahisi wa mawasiliano kwa wadau wote ili kupiga vita vitendo vya uharibifu wa Msitu.
- Kijiji kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa pembejeo za kilimo ili kupunguza kasi ya kilimo cha kuhamahama.
- Kuandaa na kutoa taarifa ya mwaka.
- Kufanya mapitio ya mpango wa usimamizi wa Msitu.

5.2 Ulinzi wa Msitu

Usimamizi na ulinzi wa Msitu wa Kijiji utakuwa chini ya Serikali ya Kijiji na ni jukumu la wanakijiji wote.

5.2.1 Ushirikishwaji wa Jamii katika Ulinzi wa Msitu

Msitu utalindwa na wanajamii wote wanaopakana na msitu. Kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa Kijiji au Kamati ya Maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya Maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za ulinzi wa Msitu.

5.2.2 Walinzi wa Doria

Kutakuwa na timu ya doria itakayopendekezwa na Halmashauri ya kijiji na baadae kuidhinishwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kikosi cha doria kitakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika Msitu wa Kijiji. Muundo wa Kikosi cha doria utakuwa kama ifuatavyo:-

- Kamanda mmoja wa kikosi.
- Wajumbe watatu wa Kamati ya Maliasili, na
- Wanakijiji wawili.

Doria inaweza kuwa ya wanakikosi wanne hadi sita, na kila doria lazima awepo mjumbe mmoja wa Kamati ya Maliasili, na mwanajamii mmoja. Kikosi cha doria kitaweka kumbukumbu zote za doria katika kitabu cha doria na kitatoa taarifa za matukio kwa Kamati ya Maliasili baada ya doria. Doria itafanyika angalau mara tatu kwa mwezi. Wanadoria watalipwa posho endapo kuna fedha na kutokana na bajeti ya Kamati ya Maliasili iliyopitishwa na Halmashauri ya Kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Kamanda wa Kikosi cha doria atapendekezwa na Halmashauri ya Kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kamanda wa kikosi cha doria atakuwa na sifa zifuatazo;

- Mtu shupavu ambaye ni mwaminifu na/au
- Awe amefudhu mafunzo ya mgambo
- Ambaye ana moyo wa kujituma na kujitolea
- Awe anafahamu vizuri maeneo ya Msitu

Wanakikosi cha doria watakaobainika kutokuwa waaminifu watafukuzwa mara moja na wengine watachaguliwa kujaza nafasi zao.

5.3 Kusafisha Mpaka na Barabara za Moto

Kamati ya Maliasili ya Kijiji na jamii kwa ujumla watashiriki katika kuandaa mpango wa kudhibiti mioto Msituni. Ubabuaji moto ni hatua mojawapo muhimu katika kudhibiti moto, na hili ni jukumu la Kamati ya Maliasili na wanajamii kwa ujumla. Zoezi la ubabuaji litatekelezwa na wanajamii wote kwa usimamizi wa Afisa misitu au wataalamu wa moto.

5.4 Kurudisha hali ya Msitu

5.4.1 Kutokana na Machipukizi (Uoto wa asili)

Njia hii hutegemea miche iliyoota yenyewe kutokana na mbegu, mashina au mizizi ya miti iliyovunwa.

5.4.2 Upandaji wa miti kwenye maeneo yaliyo wazi

Maeneo yote yaliyo wazi ndani ya msitu ambayo yanaonekana ni vigumu uoto wa asili kujaza yatapandwa miti inayokubaliana na mazingira hayo hasa ile iliyokuwepo lakini ikaadimika kutokana na matukio ya moto ya mara kwa mara na uvunaji holela uliokuwa ukifanyika kipindi cha nyuma.

5.4.3 Palizi kwenye maeneo yaliyopandwa miti

Palizi ya kisahani itafanyika mara moja kwa mwaka ili kuhakisha miche iliyopandwa haisongwi na majani au mimea mingine.

SURA YA SITA

6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU

6.1 Vyanzo vya Mapato

Kutakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo toka Msitu wa jamii:

- Ushuru
- Ada za leseni
- Ada za vikundi vilivyoko mafunzoni, shughuli za utafiti na utalii
- Faini za wahalifu
- Mauzo ya rasilimali za Msitu

6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya Msitu utakuwa kati ya Serikali ya Kijiji (95%) na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji (5%) kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa usimamizi wa Msitu na utekelezaji wa shughuli za maendeleo za Kijiji.

6.3 Matumizi ya Mapato

Mapato yatokanayo na Msitu yataelekezwa katika shughuli za;

- Kuendeleza shughuli za Msitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa Serikali ya Kijiji ili yatumike katika shughuli za jamii.

Mgawanyo wa asilimia tisini na tano (95%) ya pato la Kijiji utakua kama ifuatavyo;

- Asilimia arobaini (40%) ya pato la Kijiji itakuwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa Msitu chini ya Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

- Asilimia hamsini na tano (55%) ya pato la Kijiji litakuwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Kijiji chini ya Halmashauri ya Kijiji.

6.4 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha

Kamati ya Maliasili itakuwa na jukumu la kukusanya mapato yote yatokanayo na Msitu. Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogo madogo. Pesa ndogondogo haitakiwi kuzidi shilingi laki tatu (300,000/-). Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Nyamwage. Kutakuwa na watia sahihi wanne;

- Afisa Mtendaji wa Kijiji (A),
- Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango, Uchumi na Fedha ya Kijiji (A),
- Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili (B)
- Mweka Hazina (B) wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

Mtia sahihi mmoja wa A na mmoja wa B watahitajika kuchukua pesa toka benki.

6.4.1 Vitabu Muhimu vya Kutunza Kumbukumbu Vinavyotakiwa

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili atakuwa na jukumu la kutunza vitabu vya kumbukumbu.

Vitabu vinatakiwa kuwa tayari kwa ukaguzi wakati wowote na vitakaguliwa na;

- Kamati ya fedha na mipango ya Serikali ya Kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vitabu vitakavyokaguliwa ni;

- Jalada la kumbukumbu/muhitasari wa vikao.
- Kitabu cha kumbukumbu za doria kinachoonyesha tarehe ya doria, njia iliyotumika, kama kuna wahalifu waliokamatwa na dalili zozote za kuwepo kwa uharibifu wa Msitu.
- Kitabu cha kumbukumbu za uhalifu kinachoonyesha majina ya wahalifu, faini zilizolipwa, tarehe na nambari ya stakabadhi.
- Vitabu vya vibali na leseni vinavyoonyesha nambari ya kibali, mpewaji, sababu ya kibali, kiasi cha mzigo, kiasi cha fedha, nambari ya stakabadhi, tarehe na jina la mwanakamati aliyesimamia.
- Kitabu cha stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika kulingana na mpango huu.
- Kitabu cha matumizi madogo madogo kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya pesa ambazo hazikuwekwa katika akaunti ya benki.
- Taarifa ya Mapato na Matumizi

6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya maliasili itatoa taarifa za mara kwa mara kuonesha mwenendo wa mapato na matumizi kupitia mbao za matangazo kijijini

Kamati ya Maliasili itatoa taarifa ya Mapato na Matumizi kila mwezi kwa Halmashuri ya Kijiji. Pia kila baada ya miezi mitatu Serikali ya Kijiji itatoa taarifa ya maendeleo ya usimamizi wa Msitu, na mapato na matumizi katika mkutano mkuu wa Kijiji ambapo Kamati ya Maliasili nayo inaweza kuwasilisha taarifa au kutoa ufafanuzi wakati wa majadiliano.

6.4.3 Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha zilizotokana na Msitu atawajibishwa na Serikaliya Kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluhishi la Kata au Mahakama ya mwanzo kwa kupata ushauri kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kata au Afisa Misitu wa Wilaya. Mjumbe yeyote wa Serikali ya kijiji au Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima awajibishwe kulingana na Sheria ndogo za usimamizi wa Msitu za kijiji na ikilazimika ajiuzulu au atalazimishwa kujiuzulu haraka na uchaguzi mpya utafanyika kumchagua mjumbe mwingine kuziba pengo hilo.

SURA YA SABA

7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI

7.1 Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

7.2 Tathimini ya Kati na ya Mwisho

Zoezi la kubaini fursa na vikwazo litafanyika ili kuelewa hali ya maendeleo kama ilivyobainishwa katika mpango kazi huu. Zoezi hili litafanyika mwishoni mwa mwaka wa pili, na mwishoni mwa kipindi cha miaka mitano.

Tathimini itafanyika kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la utekelezaji wa mpango kazi lililoonyeshwa katika kiambatisho B. Zoezi hili la tathmini litaongozwa na Afisa Misitu wa Wilaya chini ya mpango wa kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu.

UHALALI WA MPANGO

MPANGO WA USIMAMIZI MISITU

Mpango huu wa Usimamizi Misitu ya Kijiji cha Nyamwage umepitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji na kuidhinishwa na Afisa Misitu wa Wilaya. Sheria Ndogo zilizoambatanishwa na mpango huu zimepitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji, Baraza la maendeleo la Kata na Baraza la Madiwani.

Mpango huu unasisitiza kuwa ni jukumu la wanakijiji wa Nyamwage kutunza, kusimamia, kutumia kiendelevu na kuendeleza msitu wao kufuatana na malengo ya mpango wa Usimamizi Msitu.

MAREKEBISHO YA MPANGO

Jamii ya Kijiji cha Nyamwage itafanya marekebisho ya jambo lolote katika mpango huu, wataomba ushauri kwa Afisa Misitu wa Wilaya ambaye atashauri na kutoa maoni juu ya marekebisho hayo. Marekebisho hayo yakikubaliwa yatatiwa saini na yataambatanishwa katika mpango huu. Kwa madhumuni ya ufanisi wa haraka wa marekebisho hayo, Afisa misitu wa Wilaya anaweza kutia sahihi kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya.

Mpango huu wa usimamizi wa msitu wa Kijiji cha Nyamwage umesainiwa na:

_____

Mwenyekiti wa Kijiji

_____

Mwenyekiti Kamati ya Maliasili

_____

……

Afisa Misitu wa Wilaya ya Rufiji

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A : *RAMANI YA MISTU WA NYAMKONGO(NYAMWAGE)*



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Kijiji cha Nyamwage. Eneo linaloonekana jeusi/kijani ni eneo ambapo uvunaji hauruhusiwi kabisa. Na pia msitu una baadhi ya maeneo yenye Misitu ya ukanda wa pwani ambayo kwenye ramani hajaonyeshwa, Vipimo vya GPS (WGS84: 37S)katika mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	**Nambari ya utambulisho**	**E (m)**	**N (m)**
1.		501484	9098588
2.		501271	9101706
3.		503183	9101635
4.		503326	9101271
5.		503909	9101051
6.		504295	9100387
7.		505194	9098686
8.		505038	9097382
9.		504781	9096835
10.		504132	9096477
11.		503802	9095975
12.		502202	9095661
13.		502144	9096449
14.		502517	9097480
15.		502404	9097729
16.		502062	9097910
17.		501839	9098266

KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI

Kila mwaka Kamati ya Maliasili ya Kijiji ni lazima iandae mpango kazi kwa mwaka unaofuata.

Kazi za Kila Mwaka

- Kuhakiki mipaka ya Msitu.
- Kusafisha mipaka ya Msitu na kulima barabara za kuzuia moto
- Kudhibiti uchomaji moto ovyo Msituni;
- Kudhibiti malisho ya mifugo Msituni;
- Kuelimisha jamii juu ya madhara ya moto kwa Misitu na viumbe vilivyopo;
- Kuhamasisha jamii kupanda miti;
- Kutoa elimu kwa Kamati ya Maliasili na kikosi cha doria;
- Kusimamia matumizi ya Sheria ndogo za Msitu (Serikali ya Kijiji);
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya Misitu (Kamati ya Maliasili);
- Kukuza ushirikiano na vijiji vingine juu ya usimamizi wa Misitu. ;
- Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza Msitu;
- Kushirikisha vijiji jirani kwenye ulinzi wa Msitu;
- Kuweka mpango mzuri kwa Kamati mpya kuwa na uwakilishi wa Kamati ya zamani;
- Kupiga vita kilimo cha kuhamahama;
- Kuwezesha urahisi wa mawasiliano kwa wadau wote ili kupiga vita vitendo vya uharibifu kwa urahisi zaidi;
- Kijiji kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa pembejeo ili kupunguza kasi ya kilimo cha kuhamahama na nyinginezo.

Kazi za Mwaka wa kwanza

- Kupaka rangi ya bluu na kuweka mabango ya alama kuzunguka mipaka ya Msitu
- Kufanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya barabara za kuingia za ndani ya Msitu na kuzitengeneza au kuziboresha
- Ujenzi wa vituo vya doria kuzunguka Msitu
- Kuandaa mpango wa kudhibiti mioto kichaa Msituni
- Kuweka alama za tahadhari za moto
- Kufanya doria
- Kutengeneza barabara za kuzuia moto;
- Kuelimisha jamii
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za usimamizi wa Msitu za robo, nusu na mwaka kwa Halmashauri ya Kijiji na kwenye Mikutano mikuu

Kazi za Mwaka wa Pili

- Kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti uvunaji holela na uharibifu mwingine wa Msitu;
- Kuelimisha jamii juu ya madhara ya moto kwa Misitu na viumbe vilivyopo;
- Kufanya mapitio ya mpango;
- Ubabuaji moto Msitu,
- Kupanda miti kwa maeneo ya mipaka na maeneo yaliyo wazi
- Kupalilia miti michanga
- Kuandaa na kutoa taarifa ya mwaka.
- Uendeshaji na uendelezaji wa miradi midogo
- Kutafuta masoko ya mazao ya Misitu
- Kusimamia uvunaji
- Kujenga kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu

Kazi za mwaka wa tatu, wa nne na watano zitapangwa kulinga na matakwa/mahitaji na vipaombele vya usimamizi wa Msitu wa Kijiji kwa kipindi hicho ambazo zitazingatia mpango huu.

Kazi za Mwaka wa Tatu

.....

Kazi za Mwaka wa Nne

.....

Kazi za Mwaka wa Tano

……

KIAMBATISHO C : VIWANGO VYA USHURU

Shughuli zifuatazo zitatozwa ushuru kwa Serikali ya Kijiji kama ifuatavyo;

- Ziara ya mafunzo ni shilingi 20,000/- kwa kichwa kwa Mtanzania na shilingi 25,000/- kwa mgeni toka nje ya Nchi kwa siku.
- Kufanya utafiti wa kibiashara au kampuni ni shilingi 100,000/- kwa wiki, wanafunzi wa kitanzania shilingi 30,000/- na wanafunzi wasio watanzania shilingi 50,000/- kwa wiki na nakala moja ya taarifa ya utafiti itabaki Kijijini. *Endapo tafiti hizi zitakuwa zikihususha uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na uvunaji wa rasilimali za Msitu, tathimini ya uharibifu huo au uvunaji itafanyika na mtafiti atalazimika kulipia gharama za uharibifu huo.*
- Watalii wa kigeni watalipa shilingi 25,000/- kwa siku kwa kichwa na watalii wa ndani watalipa 20,000/= kwa siku kwa kichwa.
- Waongoza watalii na wageni watalipwa shilingi 10,000/- kwa siku kwa kichwa.
- Majengo -Nguzo shilingi 5,00/= kwa kila moja; Mapau shilingi 300/= kwa kila moja; Fito shilingi 500/= kwa mzigo wenye fito thelathini.
- Kuni kwa ajili ya biashara shilingi 3,000/= kwa kila mita moja ya ujazo.
- Vyakula na matunda shilingi 3,000/= kwa ndoo ya plastiki.
- Kutundika mizinga ni shilingi 5,000/= kwa kila mzinga kwa mwaka.
- Kuchuma majani ya dawa shilingi 5,000/= kwa kiroba (kilo 50) ; magome na mizizi ni shilingi 3,000/= kwa kilo.
- Miti ya vifaa vya nyumbani kwa biashara

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA WILAYA (SURA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 168

SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI, USIMAMIZI, NA UTUMIAJI RASILIMALI ZA MISITU YA NYAMKONGO) HALIMASHAURI YA KIJIJI CHA NYAMWAGE

Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika

1 Sheria hizi zitaitwa sheria ndogo za (utunzaji, usimamizi na utumiaji wa Rasilimali za Msitu ya Nyamkongo) za Halmashauri ya Kijiji cha Nyamwage za mwaka 2016, na zitaanza kutumika mara baada kupitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Rufiji Mwaka11/2006

Eneo la Kutumika

2 Sheria ndogo hizi zitatumika kwenye eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Kijiji cha Nyamwage .

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Halmashauri ya Kijiji" maana yake wajumbe wasiopungua 15 na wasiozidi 25 wa Halmashauri ya Kijiji, kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982

"**Kamati ya Maliasili ya Kijiji"** Maana yake ni Kamati iliyochaguliwa na kuundwa na Serikali ya Kijiji kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji ambayo majukumu yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu Msitu iliyopo ndani ya mipaka na maliasili nyingine zilizomo kwenye Kijiji;

"Kijiji" maana yake ni Kijiji cha Nyamwage pamoja na Vitongoji vyake ;

"Kiongozi" Mtu yeyote aliyepewa madaraka na mamlaka na wananchi ili awatumikie.

"**Madini**" maana yake ni madini ya vito, shaba, almasi, na ni pamoja na madini ya ujenzi ambayo ni mawe, kokoto, mchanga na kifusi; kama ilivyoainishwa katika sheria ya Madini ya mwaka 2010

"Meneja wa Msitu " maana yake ni Kamati ya Maliasili ambayo kazi yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu Msitu wa Kijiji;

" Misitu wa Kijiji''maana yake ni eneo la Msitu lililotengwa na Kijiji lenye miti na uoto mwingine wa asili linalomilikiwa na Kijiji cha Nyamwage, kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Usimamizi

wa Msitu wa Kijiji wa mwaka 2016-2020 ;

"**Mkurugenzi**" ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji pamoja na mtu yeyote aliyeidhinishwa kufanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, (Mamlaka za wilaya) ya mwaka 1982

"Mkutano mkuu wa Kijiji" maana yake ni mkutano wa wananchi wa Kijiji cha Nyamwage, kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa, (Mamlaka ya Wilaya) ya 1982

"Mpango wa Usimamizi wa Misitu" maana yake ni kabrasha lenye maelezo ya namna jamii ya Kijiji itakavyokuwa inatunza, kusimamia na kutumia rasilimali za Msitu wa Nyamwage;

"**Mwanakijiji"** Maana yake ni mtu yeyote aliyeandikishwa kwenye orodha ya daftari la wakazi kwa ajili ya kuwa mwanakijiji;

"**Sheria**"- Maana yake ni sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tamko, mwongozo au kanuni yoyote iliyotolewa na serikali na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali

Utaratibu wa jumla wa kutumia Msitu na mazao ya Msitu

4 UTARATIBU WA JUMLA WA KUTUMIA MSITU NA MAZAO YA MSITU

1 Watu ambao wanaruhusiwa kuingia katika Msitu wa Kijiji kwa shughuli mbalimbali za usimamizi kutokana na taratibu zilizokubalika ni wakazi wa Kijiji cha Nyamwage tu;

2 Watu wengine kutoka nje ya Kijiji cha Nyamwage wataruhusiwa kuingia ndani ya Msitu wa Kijiji kwa vibali maalum;

3 Kwa wale wanakijiji wasiojiweza ambao wanatambuliwa na Serikali ya Kijiji kama vile wagonjwa wa kudumu, walemavu na wazee watachukua mazao ya Msitu yasiyo ya biashara bure bila kutozwa ushuru wa aina yeyote;

4 Kwa mazao ya matumizi ya nyumbani kama vile matunda pori, vyakula pori, mbogamboga, kuni kavu, madawa na ukindu yatavunwa bure siku maalum itakayopangwa na mkutano mkuu wa Kijiji, siku hiyo inaweza kubadilika kutokana na matakwa ya jamii.

5 Wanajamii wote wa Kijiji cha Nyamwage watakaohitaji mbao kwa ajili ya ujenzi watalipia asilimia hamsini (50%) kwa kila mita moja ya ujazo pungufu ya bei iliyoelekezwa na Serikali na itafanyiwa marekebisho wakati wa kurekebisha mpango wa usimamizi wa Msitu . Fursa hiyo ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba Kijijini Nyamwage tu.

Uvunaji wa mazao ya Msitu kibiashara

5 UVUNAJI WA MAZAO YA MSITU KWA AJILI YA BIASHARA

Mazao yote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatavunwa kwa kulipia ushuru na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002**.**

Masharti ya matumizi ya Msitu na mazao ya Msitu wa kijiji

6 MASHARTI YA MATUMIZI YA MSITU NA MAZAO YA MSITU WA KIJIJI

Bila kuathiri masharti mengine yaliyotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi matumizi ya Msitu na mazao ya Msitu wa Nyamwage itakuwa kama ifuatavyo:-

i. **Matumizi yaliyoruhusiwa bila kibali wala ushuru ni:-**

   a. Kuchota maji,

   b. Kufanya matambiko bila kuathiri mazingira,

   c. Njia za miguu na barabara za kukatiza Msitu kama kutakuwa na ulazima.

ii. Matumizi yaliyoruhusiwa kwa vibali maalum bila malipo ni kwa matumizi ya nyumbani kwa wakazi wa Nyamwage:-

   a. Kukusanya matundapori, mbogamwitu,uyoga, kuokota kuni (miti mikavu tu), kukata miyaa, kuchimba viazi pori,upekecho.

   b. Kutumia mazao ya Misitu kwa ajili ya maendeleo ya huduma za jamii .

iii. Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kulipiwa vibali au leseni

   a. Kuvuna miti ya majengo kwa ajili ya biashara;

   b. Kuvuna mbao na magogo.

iv. Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kulipiwa ushuru/ada

   a. Utafiti;

   b. Utalii;

   c. Kutundika mizinga na urinaji wa asali kwa watu binafsi au vikundi visivyo vya Kijiji

   d. Mafunzo ya vikundi.

Bila kuathiri kifungu kidogo cha (iii) (a na b) hapo juu utaratibu wa kuvuna magogo na mbao ni ule uliowekwa na Sheria ya Misitu.

v. Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu

   a. Kuchoma moto ovyo Msitu ;

   b. Kukata na kupasua miti ambayo haikuorodheshwa kwenye Mpango wala kufanyiwa tathmini;

c. Kutega wanyama pori;

d. Kuharibu uoto wa asili sehemu yeyote katika Msitu ;

e. Kurina asali kwa kutumia moto;

f. Shughuli za kilimo;

g. Makazi ya watu;

h. Kuchoma mkaa bila kufuata utaratibu uliokubaliwa na Kijiji;

i. Kuchunga mifugo;

j. Kurina asali kwa kuangusha miti kunakojulikana kama kubangua asali.

k. Kuchuna kamba kwenye miti iliyo ndani ya Msitu wa Kijiji.

MUHIMU:Mtu yeyote atakayethibitika kuvunja sheria hii atatozwa faini isiyozidi 50,000/-pamoja na fidia ya uharibifu akishindwa kulipa atapelekwa mahakamani.

vi. Matumizi mengine ya Msitu yatalipiwa kama ifuatavyo.

a) Ziara ya mafunzo kwa kichwa ni shilingi 25,000/- kwa mgeni nje ya Nchi kwa siku na shilingi 20,000 kwa Mtanzania

b) Kufanya utafiti wa kibiashara au kampuni ni shilingi 100,000/- kwa wiki, wanafunzi wa kitanzania shilingi 30,000/- na wanafunzi wasio watanzania shilingi 50,000/- kwa wiki na nakala moja ya taarifa ya utafiti itabaki Kijijini. *Endapo tafiti hizi zitakuwa zikihususha uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na uvunaji wa rasilimali za Msitu, tathimini ya uharibifu huo au uvunaji huo itafanyika na mtafiti atalazimika kulipia gharama za uharibifu huo.*

c) Watalii wa kigeni watalipa shilingi 25,000/- kwa siku kwa kichwa na watalii wa ndani watalipa 20,000/= kwa siku kwa kichwa.

d) Waongoza watalii na wageni watalipwa shilingi 10,000/- kwa siku kwa kichwa.

e) Majengo -Nguzo shilingi 500/= kwa kila moja; Mapau shilingi 250/= kwa kila moja; Fito shilingi 7,500/= kwa mzigo wenye fito thelathini.

f) Kuni kwa ajili ya biashara shilingi 3,000/= kwa kila mita moja ya ujazo.

g) Vyakula na matunda shilingi 1,000 kwa kapu la wastani.

h) Kutundika mizinga ni shilingi 5,000/= kwa mz

7 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI

i. Litakuwa ni jukumu la Kijiji kutoza faini, kutoa vibali na kutoa uamuzi kwa shughuli zote zinazohusu sheria ndogo hizi. Halmashauri ya Kijiji inaweza kuagiza baadhi au shughuli zote hizi kwa Kamati ya Maliasili ya kijiji au ikibidi kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji, Kamati au Afisa Mtendaji aliyeagizwa atawajibika kwa Halmashauri ya Kijiji ambayo nayo itawajibika kwa Mkutano mkuu wa Kijiji.

ii. Vibali vyote vitatolewa na Kamati ya Maliasili na kukaguliwa na Halmashauri ya Kijiji. Lazima kibali kiwe na mhuri wa Serikali ya Kijiji pia kieleze mahali na muda mazao yatakapovunwa, idadi au kiasi na aina ya mazao hayo. Baada ya mazao kuvunwa, kupimwa, nakala moja ya kibali itabaki ofisi ya Serikali ya Kijiji.

iii. Kamati ya Maliasili kitaalam ndiyo Meneja wa usimamizi wa Msitu . Kamati hii itadumu madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3). Hata hivyo wajumbe wa kamati wanaweza kusitishwa na kukoma kuwa wajumbe endapo wataonekana kutofuata maadili ya Kamati ya Maliasili. Kamati ya Maliasili kiutendaji imeanza kazi tarehe 16/11/2006. Angalau nusu ya wajumbe waliofanya vizuri katika kipindi hicho cha miaka mitatu wabaki katika Kamati kwa ajili ya kuwapa uzoefu wajumbe wapya waliochaguliwa.

iv. Wajumbe wa Kamati ya Maliasili watateuliwa au kubadilishwa na Halmashauri ya Kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

v. Faini zitakazotozwa, mali au mapato yatakayotokana na mauzo ya mali itakayotaifishwa zitagawanywa kama ifuatavyo; Asilimia kumi (10%) atapewa mwanakijiji au wanakijiji watakaowezesha kupatikana kwa mhalifu. Asilimia tisini (90%) iliyobaki itakuwa mali ya Kijiji. Mgawanyo huu utafanyika baada ya kutoa gharama zilizotumika kuingiza mali au mapato hayo.

vi. Lazima itolewe stakabadhi kwa ada zote, faini na mali zote zitakazotaifishwa.

vii. Kiongozi au mwanakijiji yeyote wa Kijiji cha Nyamwage anayo mamlaka ya kumkamata mtu yeyote anayefanya kosa kinyume na sheria ndogo hizi na kumfikisha katika Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maliasili.

viii. Ni wajibu wa kila mwanakijiji kutoa taarifa ya ukiukwaji wa sheria hizi kwa uongozi wa Kijiji.

ix. Shughuli zote za kutunza, kusimamia na kutumia Msitu wa Kijiji cha Nyamwage zitafanywa kufuatana na mpango wa

usimamizi wa Msitu uliokubalika na jamii ya Kijiji cha Nyamwage.

8 DORIA

i. Kutakuwa na kikosi cha doria kitakachokuwa na Kamanda mmoja wa kikosi, wanakamati watatu na Wanajamii wawili wa jinsia zote wenye uelewa wa mipaka ya Msitu wa Kijiji.

ii. Doria inaweza kuwa ya wana kikosi wanne hadi sita na kila doria lazima awepo mjumbe mmoja wa Kamati ya Maliasili, na Mwanajamii mmoja.

iii. Kikosi cha doria kitaweka kumbukumbu zote za doria katika kitabu cha doria na kitatoa taarifa za matukio kwa Kamati ya Maliasili mara tu baada ya doria.

iv. Doria itafanyika angalau mara tatu kwa Mwezi. Wanadoria watalipwa posho kutokana na makubaliano yatakayofanyika na Serikali ya Kijiji.

v. Kamanda wa kikosi cha doria atapendekezwa na Halmashauri ya Kijiji kwa kufuata sifa zilizowekwa na kupitishwa na mkutano mkuu wa Kijiji

vi. Kamanda wa kikosi cha doria atakuwa na sifa zifuatazo; mtu shupavu au awe ameshiriki mgambo, moyo wa kujitolea, mwenye kujua mapori na ambaye ni mwaminifu. Kamanda wa kikosi atabadilishwa kila baada ya muda wa miaka mitatu baada ya kamati kumaliza muongo au wakati wowote pale itakapolazimu kufanya hivyo kama ilivyopitishwa na mkutano wa Kijiji tarehe **11/11/2016**

vii. Wanakikosi cha doria watakaobainika kutokuwa waaminifu wataondolewa mara moja na wengine watachaguliwa kujaza nafasi zao.

Adhabu na Makosa

9 MAKOSA NA ADHABU

i. Mtu yeyote atakayepatikana analima, kuchoma mkaa, kuweka makazi, kuchoma Misitu ovyo, kubangua asali, kuchimba madini au kukata kuni bila kibali atakuwa ametenda kosa chini ya sheria ndogo hizi na atalipa faini kwa kila kosa Shilingi elfu hamsini (50,000/=) na vifaa vyote vilivyotumika vitakuwa mali ya Kijiji na kulipia fidia ya uharibifu uliofanyika au atashtakiwa mahakamani.

ii. Mtu yeyote atakayekutwa anavuna au atakayekamatwa na magogo au mbao atalipa faini ya Shilingi elfu hamsini (50,000/=) na majengo au nguzo kwa ajili ya biashara bila ya kibali atalipa faini shilingi elfu thelathini (30,000/=) na vifaa na mali itakuwa mali ya Kijiji au atapelekwa mahakamani.

iii. Mtu yeyote akipatikana anaondoa au kubadili alama za mipaka ya Msitu zilizowekwa atakuwa ametenda kosa na atalipa faini shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kurudishia

alama zote kwa gharama zake au kupelekwa mahakamani.

iv. Mtu yeyote akipatikana na hatia ya kuchimba mawe, mchanga au udongo ndani ya Msitu atalipa faini shilingi elfu hamsini (50,000/=) na vifaa vilivyotumika kuwa mali ya Kijiji au atapelekwa mahakamani.

v. Mtu yeyote akipatikana na hatia ya kuingia Msituni bila utaratibu maalum kwa ajili ya kuchukua dawa za tiba, matunda, miyaa, ukindu, fito, kongowele, udongo, nyasi, miswaki, pikicho au mboga kwa ajili ya matumizi ya nyumbani tu atalipa faini kwa kila kosa shilingi elfu tano (5,000/=) na kupewa onyo kali.

vi. Kuchunga mifugo ndani ya Msitu faini kwa kila mnyama shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa Ng'ombe,Mbuzi na Punda. Shilingi elfu tano (5,000/=) kwa Kondoo..Kwa kipindi chote mifugo hiyo itakuwa chini ya mamlaka ya serikali ya kijiji na mmiliki wa mifugo hiyo atalazimika kulipia gharama za uharibifu utakaojitokeza. Akikaidi atafikishwa mahakamani.

vii. Wachukuzi watakaokamatwa na mazao ya Msitu watatozwa faini Kama ifuatavyo:- kwa kichwa shiling elfu mbili mia tano (2,500/=), kwa baiskeli shilingi elfu tano (5,000/=), kwa pikipiki shilingi elfu kumi (10,000/=) na kwa gari shilingi elfu hamsini (50,000/=) na mali kutaifishwa au atapelekwa mahakamani.

viii. "Kiongozi" akipatikana na hatia ya kuhusika katika kukiuka mojawapo ya taratibu zilizowekwa na sheria hii faini yake ni shilingi elfu hamsini (50,000/=), kurudisha gharama pamoja na kulazimika kujiuzulu madaraka aliyonayo au atapelekwa Mahakamani.

ix. Kama kiongozi atathibitika kuona, kusikia au kufahamu uhalifu unafanyika na kuunyamazia kimya fani yake ni shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kuondolewa madarakani au atapelekwa mahakamani.

x. Kama mtu yeyote ataizuia kamati kufanya kazi zake kwa kutishia au kutoa maneno ya kashfa atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) au atafikishwa mahakamani.

xi. Mtu yeyote ambaye ataenda kinyume na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kujaza fomu ya kukiri makosa kama zitakavyo andaliwa na Kijiji kabla ya kulipa faini.

xii. Mtu yeyote katika sheria ndogo hizi ambaye atakataa kulipa faini au kujaza fomu ya kukiri makosa atafikishwa mahakamani.

xiii. Vitu vyote vitakavyokamatwa kutokana na makosa yaliyotajwa katika vifungu (i-vii) vitataifishwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Kijiji na fedha zitakazopatikana zitakuwa mali ya Kijiji.

xiv. Bila kuathiri kifungu kidogo cha 13 (xiii) endapo mbao na

magogo vitakuwa vimekamatwa Kijiji kitatakiwa kipate ruhusa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ndani ya siku thelathini (30) kabla ya kuuza au kutumia vitu hivyo.

xv. Mtu yeyote akipatikana na hatia ya kuwinda wanyama au uvuvi wa samaki bila kibali Kijiji kitawasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya kwa hatua zaidi kama zilivyo katika sheria ya Wanyama pori na uvuvi

xvi. Endapo mhalifu yeyote atakuwa amekamatwa na mnyama/nyama pori, Kijiji kitatakiwa kuwasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya mara baada ya kumkamata mhalifu kwa hatua zaidi kama zilivyo katika sheria ya Wanyama pori.

xvii. Mtuhumiwa yeyote atakayefikishwa mahakamani na kutiwa hatiani atalipa asilimia mia moja (100%) ya gharama za kesi.

10. Matumizi ya kifungu chochote ya sheria ndogo hizi yakileta utata, sheria mama ya Misitu na wanyama pori itatumika baada ya kupata ufafanuzi, maelekezo ya kitaalam na ushauri wa kisheria kutoka kwa Mkurugenzi

Mpango wa usimamizi wa Msitu na sheria ndogo hizi zimeboreshwa na kupitishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Nyamwage uliofanyika tarehe 11/11/2016

Jina la Mwenyekiti wa kijiji.....

Sahihi.....

Tarehe.....

Jina la Mtendaji wa Kijiji .....

Sahihi.....

Tarehe.....

Mpango wa usimamizi wa msitu na sheria hizi zilipitishwa na Baraza la Maendeleo la Kata ya Mbwara (WDC) uliofanyika tarehe 22/10/2006

Sheria ndogo hizi zimepitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji uliofanyika tarehe 29/11/2006

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

Sahihi .....

Tarehe.....

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

Sahihi .....

Tarehe .....